



12 Yusufu katika Misri

Marejeo

Mwanzo 39 - 41

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yusufu aliamini Mungu hata alipokuwa gerezani. Mungu alitimiza sababu zake ndani ya maisha ya Yusufu

Maneno maalum

- 1 Yusufu mtumwa + Potifa mtu mzuri + Yusufu msimamizi
- 2 Mke wa Potifa + uongo + gereza
- 3 Mungu ana Yusufu + Yusufu msimamizi + mnyweshaji I muokaji watishwa na ndoto
- 4 Ndoto + matawi matatu + kikombe + cha zabibu + siku tatu
- 5 Ndoto + vikapu vitatu + siku tatu + nyongwa (uawa)
- 6 Farao aota + mnyweshaji anakumbuka + Yusufu anazungumzia yajayo + miaka mizuri 7 + miaka mbaya 7
- 7 Kusanya vyakula + weka galani + Yusufu msimamizi wa Misri

Maswali

1. Nani alinunua Yusufu kama mtumwa?
2. Nani alisema uongo juu ya Yusufu?
3. Nani alimfanya Yusufu awe msimamizi wa gereza?
4. Mnyweshaji aliota nini?
5. Muokaji aliota nini?
6. Mnyweshaji alikumbuka Yusufu lini?
7. Yusufu alimwambia Farao afanye nini kwa hio miaka saba mizuri?
8. Nini itafanyika kwa hio miaka saba mbaya?
9. Farao alifanya nani awe msimamizi wa Misri?
10. Farao alimpa Yusufu nini?

Majibu

1. Potifa alinunua Yusufu kama mtumwa.
2. Mke wa Potifa alisema uongo juu ya Yusufu.
3. Mkuu wa gereza alimfanya Yusufu msimamizi wa gereza.
4. Ndoto za mnyweshaji ilikuwa juu ya mzabibu na matawi tatu ya zabibu zilizokamuliwa ndani ya kikombe cha Farao.
5. Ndoto za Muokaji ilikuwa juu ya chakula ndani ya vikapu vitatu juu ya kichwa chake na ndege walikuja na kula hicho chakula.
6. Mnyweshaji alimkumbuka Yusufu wakati Farao aliota ndoto.
7. Yusufu alimwambia Farao aweke chakula kingi kwa hiyo miaka saba mizuri.
8. Kwa miaka 7 mbaya, kutakuwa na njaa sana
9. Farao alifanya Yusufu kuwa msimamizi wa Misri yote
10. Farao alimpa Yusufu Pete, Vazi na Mkufu wa Dhahabu

12.1 Yusufu alikuwa mtumwa Misri. Alinunuliwa na Potifa mkuu wa askari wa Farao. Potifa alikuwa mtu mzuri, alimwamini Yusufu na alimfanya msimamizi juu ya kila kitu chake.

12.2 Lakini mke wa Potifa alikuwa mmbaya na akasema uongo juu ya Yusufu. Akamkasirisha Potifa akamueka Yusufu gerezani lakini Mungu alikuwa na Yusufu.

12.3 Mkuu wa gereza alimueka Yusufu kama msimamizi wa wafungwa wote. Kulikuwa na wafungwa wawili, mnyweshaji na muokaji wa Farao. Usiku mmoja wote wawili waliota ndoto zilizowatisha.

"Hizi ndoto zina maana gani?" walimuuliza Yusufu. "Mungu atatafsiri maana ya hizo ndoto," Yusufu alisema.

12.4 "Niliota juu ya mzabibu," mnyweshaji alisema, "kulikuwa na matawi matatu juu ya huo mzabibu na vishada (vifungu) vya zabibu. Kikombe cha Farao kilikuwa mkononi mwangu, nikazikamulia mzabibu ndani ya hicho kikombe. Nikampa Farao.



"Matawi matatu ni siku tatu," Yusufu alisema, "baada ya siku tatu, Farao atakurudisha uwe mnyweshaji tena na uendelee kumpa divai yake." Mnyweshaji alifurahi sana.

"Mwambia Farao juu yangu ili nitoke hapa gerezani," Yusufu alisema

12.5 "Hata nami nilikuwa na ndoto," Muokaji alisema. "Nilikuwa na vikapu vitatu juu ya kichwa changu. Ndani ya kikapu kimoja cha juu kulikuwa na chakula cha Farao, lakini ndege walikula hicho chakula."

"Kwa siku tatu," Yusufu alisema, "Farao atakunyonga kwa mti, na ndege watakukula." Ilifanyika tu, vile Yusufu alisema, baada ya siku tatu Farao alimrudishia mnyweshaji kazi yake lakini Muokaji alinyongwa kwa mti na ndege wakamla.

12.6 Mnyweshaji alirudi kwa Jumba la Kifulme ya Farao lakini alimsahau Yusufu. Baada ya miaka mitatu, farao alipata ndoto, ndio mnyweshaji akamkumbuka Yusufu.

"Ninajua mtu anayeweza kutafsiri ndoto," alisema. "Nilipokuwa gerezani, niliota ndoto na kijana mwebrania aliniambia maana yake."

Farao aliamrisha Yusufu aletwe. Farao alimwambia Yusufu ndoto zake. "Mungu amekwambia chenye atafanya," Yusufu alisema. "Kutakuwa na miaka saba ya mavuno mengi hapa Misri, baadaye kutakuwa na miaka saba ya njaa kuu na hakuna kitakachomea."

12.7 Yusufu alimwambia Farao achague mtu mzuri mwenye hekima ili asimamie Misri kwa kukusanya chakula wakati wa miaka saba ya mavuno mengi.

"Weka nafaka kwa kila mji," Yusufu alisema, "Weka kwa ajili ya hizo miaka za njaa nyingi." Farao alifurahi kwa kusikia maana ya hizo ndoto. "Tunaweza kumpata mtu mwenye hekima kuliko wewe?" Farao alisema. "Nitakuweka wewe uwe msimamizi wa nchi nzima ya Misri.

Farao alitoa pete kutoka kwa kidole chake na kumvalisha Yusufu, akampa nguo za kitani na mkufu wa dhahabu ya shingo. Kwa hivyo, Yusufu alisimamia nehi yote ya Misri.